# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI

Mamlaka ya Usafiri Baharini imeanzishwa chini ya sheria namb. 3 ya mwaka 2009. (Zanzibar Maritime Authority, Act No. 3 of 2009), na inafanya kazi zake za kila siku chini ya sheria ya Usafiri Baharini (Maritime Transport Act No. 5 of 2006).

Mamlaka ya Usafiri Baharini – Zanzibar inatangaza nafasi za kazi kwa kada mbalimbali kama ifuatavyo:-

**1.1 AFISA MKAGUZI WA MELI DARAJA LA II "Nafasi (6)"**

**1.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- **i.** Kukagua meli na kujiridhisha kuwa ziko katika kiwango cha usalama na kuwasilisha ripoti kwa Mkuu wa kazi;
- **ii.** Kukagua na kuthibitisha taarifa za nyaraka za meli na Wafanyakazi wake;
- **iii.** Kukagua vyombo vyote vya baharini kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo;
- **iv.** Kuweka kumbukumbu ya meli zilizokaguliwa, zilizo kizuizini na taarifa nyengine zinazohusiana na ukaguzi huo;
- **v.** Kufanya uchunguzi na kukusanya taarifa zitakazotumika katika uchunguzi wa ajali na
- **vi.** Kufanya kazi nyengine yoyote atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**1.3 Sifa za Muombaji:**

Awe mwenye cheti cha umahiri daraja la II (Certificate of Competence Class II) na kuendelea; au mwenye elimu ya Shahada ya kwanza na kuendelea katika fani ya Masuala ya Baharini/ Usafirishaji wa Baharini/ Usanifu wa Majini/Usalama wa Baharini/ Uhandisi wa Meli, au fani inayolingana na hiyo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### 1.4 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali ZPSH-04

### 2.1 AFISA USAJILI WA MELI DARAJA LA II “NAFASI (2)”

### 2.2 MAJUKUMU YA KAZI

- **i.** Kukusanya taarifa za uzito wa meli zilizokubaliwa kusajiliwa;
- **ii.** Kukusanya taarifa za maombi ya usajili wa meli na kuangalia kama zinafaa kusajiliwa;
- **iii.** Kuandaa utaratibu wa malipo yanayohusiana na usajili na hati za meli;
- **iv.** Kuhifadhi kumbukumbu za meli zilizosajiliwa na kupewa hati;
- **v.** Kufuatilia nyenendo za meli ili kuhakikisha zina sifa za kubaki katika usajili na na
- **vi.** Kufanya kazi nyengine yoyote atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

### 2.3 Sifa za Muombaji:

Awe mwenye elimu ya Shahada ya kwanza na kuendelea katika fani ya Usafirishaji wa Baharini/ Usalama wa Baharini/ Elimu na mafunzo ya baharini/ Uhandisi wa Meli, au cheti cha umahiri daraja la III (Certificate of Competence Class III) au fani inayolingana na hiyo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### 2.4 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali ZPSH-04

### 3.1 MSAIDIZI USALAMA WA MELI DARAJA LA III ‘’ Nafasi (1) ‘’

### 3.2 MAJUKUMU YA KAZI

- **i.** Kusaidia uzingatiwaji wa muda na taratibu za meli/ chombo wakati wa kuondoka na kuingia;

ii. Kusaidia kusimamia usalama wa abiria, mizigo na mali zao wakati wa kuingia na kutoka melini;

iii. Kusimamia taratibu zitakazohakikisha kuwa ngazi ya kuingilia na kutokea katika chombo imewekwa vizuri na kuwekewa nyavu ya usalama pembeni;

iv. Kusimamia kuwa chombo kinachukuwa abiria kwa mujibu wa idadi iliyopangiwa;

v. Kusaidia kupokea malalamiko ya abiria na kuwasilishwa kwa mkuu wa kazi;

vi. Kusaidia kukusanya taarifa kwa ajili ya uwekaji kumbukumbu ya abiria wote waliomo katika chombo/ meli kinachokuja na kuondoka;

vii. Kusaidia kudhibiti mwenendo wa makuli katika chombo;

viii. Kusaidia kutoa taarifa ya tukio lolote kuhusiana na usalama na ulinzi wa chombo na abiria na

ix. Kufanya kazi nyengine yoyote atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**3.3 Sifa za Muombaji:**

Awe mwenye elimu ya cheti katika fani ya Masuala ya Baharini/ Usafirishaji wa Baharini/ Usalama wa Baharini/ Elimu ya Mafunzo ya awali ya Baharini, "Basic Mandotary Certificate" au fani inayolingana na hiyo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**3.4 NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali ZPSE-02

**Jinsi ya Kuomba:-**

- Barua za maombi ziandikwe kwa Mkono kwa anuani ifuatayo:-
  **MKURUGENZI MKUU**
  **MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI**
  **S.L.P 401, - ZANZIBAR**
- Muombaji anatakiwa kuwasilisha ombi lake moja kwa moja Mamlaka ya usafiri Baharini iliyopo Bohari Kuu - Malindi Zanzibar wakati wa saa za kazi.

Barua za maombi ziambatanishwe na mambo yafuatayo: -

a) Kivuli cha Cheti cha kumalizia masomo
b) Kivuli cha Cheti cha mtihani wa Taifa (Elimu ya Sekondari)
c) Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa
d) Kivuli cha Kitambulisho cha Mzanzibar.
e) Picha moja (1) ya Passport Size iliyopigwa karibuni.
f) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
g) Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
h) Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**
i) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

j) Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni **tarehe 25 Novemba, 2022** wakati wa saa za kazi.

- Muombaji anatakiwa aainishe nafasi ya kazi anayoiomba kati ya zilizotajwa hapo juu vinginevyo maombi yake hayatazingatiwa. Kwa waombaji walioko Pemba wanaombwa kuwasilisha maombi yao katika Ofisi ya Mamlaka ya Usafiri Baharini iliyopo Mkoani Pemba.

***PIA TANGAZO HILI LINAPATIKANA KATIKA TOVUTI YA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI AMBAYO NI*** www.zma.go.tz